TanzaniaDaima
Jumapili, Machi 15, 2020

JS

# JAHAZI LA SIASA

Baruapepe: tanzaniadaima@gmail.com

Nani mkweli kuhusu amani ya Tanzania?

UK 10



Matunda ya programu ya urithi ukombozi wa Afrika

UK 11



# Waziri Mkuu amepotoshwa?

NA SADIK SADIK, TANGA

KWANZA natangaza masilahi kwamba mimi ni mdau na mkulima mkubwa wa mkonge wa miaka mingi, naijua vizuri historia ya kampuni ya Katani na sintofahamu inayoendelea sasa.

Naandika hii kutokana na ripoti ya uchunguzi wa Tume iliyoundwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa ambayo binafsi nimebaini kuna ukweli uliofichwa ama kwa bahati mbaya au kusudi.

Kampuni ya Katani Limited iliundwa wakati wa mchakato wa ubinafsishwaji wa shirika lililojulikana TANZANIA SISAL AUTHORITY (TSA) (MAMLAKA YA MKONGE TANZANIA) (MMT).

Katani Limited ilishinda zabuni na kununua hisa 999,999 kati ya hisa 1,000,000 za Kampuni ya MGC (sehemu ya TSA/MMT) zilizouzwa na The Presidential Parastatal Sector Reform Commission (PSRC).

Katani Limited ni kampuni ya uwekezaji na uongozi (Investment & Management Company) ambayo ilikuwa inamilikiwa na wanahisa watatu.

Kulikuwa na wawekezaji wa nje ambao kwa pamoja walimiliki asilimia 90 ya hisa za Katani Limited.

Wawekezaji hao ni Grecian Investment (UK) Ltd, ambayo mmiliki wake ni raia wa Kigiriki na aliwahi kuwa mkulima wa mkonge Tanzania.

Pili ni Wigglesworth & Co Ltd, ya Uingereza ijulikanayo duniani kama wanunuzi, wauzaji na wasambazaji wakubwa wa mkonge na bidhaa zake. Kampuni hii imekuwa inafanya shughuli hizi kwa zaidi ya miaka 105.

Na mwekezaji wa tatu ni Dekowe GmbH ya Kijerumani inayotengeneza, kusambaza na kuuza mazulia ya mkonge, Amerika ya Kaskazini, Ulaya, Japani na Bara la Asia. Pia ina viwanda Portugal, Romania na India. Kampuni hii imekuwa ikifanya shughuli hizi kwa zaidi ya miaka 120.

INAENDELEA UK.12

Scanned with CamScanner

Baruapepe: tanzaniadaima@gmail.com



Baruapepe: tanzaniadaima@gmail.com



# Waziri Mkuu amepotoshwa?

INATOKA UK. 9

Umoja wa wafanyakazi 87 akiwemo Salum Shamte na wenziwe 86 walikuwa wataalamu waajiriwa wa ofisini na mashambani. Hao kupitia mafao yao kwa pamoja waliweza kulipia asilimia 10 ya hisa za Katani Ltd, kupitia kampuni waliyoisajili na ilijulikana kwa jina la Mkonge Investments and Management Co. Ltd (MIM).

Hivyo, Katani Limited iliingia mkataba na Serikali wa kununua baadhi ya mali hizo za TSA (ambazo zilihamishiwa kwenye kampuni ya MGC), Februari 13, 1998.

**MKATABA WA MAUZO:**

Wawekezaji hao wanne kwa ujumla wao walilipa malipo ya awali na kuanza uwekezaji kama ilivyo kwenye mkataba.

Hali ya mashamba na mitambo kabla ya kuanza uwekezaji ilikuwa mbaya sana;

Chini ya TSA (ambalo lilikuwa ni Shirika la Umma lililopewa dhamana ya kusimamia na kuendesha shughuli za mkonge baada ya utaifishaji), uzalishaji wa mkonge ulishuka kutoka tani 234,000 mwaka 1964 hadi 19,000 mwaka 1997;

Miundombinu ilikuwa imechakaa na kuharibika, mashine zilikuwa zimechakaa na mitambo ilikuwa mibovu;

TSA ilikuwa imetengeneza hasara kwa zaidi ya miaka 15 kabla ya kubinafsishwa.

Mchakato wa ubinafsishaji ulichukua takribani miaka 6 kabla ya kukamilika Februari 1998.

Kipengele muhimu kwenye mkataba wa mauzo ni upatikanaji wa hati za mali zilizohamishiwa MGC kutoka TSA, ambazo Serikali iliahidi kuzitoa ndani ya miezi sita.

Uwekezaji ulianza mara moja kwa wawekezaji kutumia fedha zao.

Kiwanda cha TANCORD, kilichokuwa kimefungwa, kilifanyiwa ukarabati na ndani ya miezi saba tu kilianza kazi.

UKIUKWAJI WA MAKUBALIANO

Wawekezaji walifuatilia hati hizo kwa muda wa miezi 22 bila mafanikio; Hati zilikuwa ni nyenzo muhimu kwa wawekezaji kutafuta mitaji na mikopo ndani na nje ya nchi.

Desemba 1998 wawekezaji wa nje walisimamisha utoaji wa fedha zao na Desemba 1999 waliamua kuondoka na kuuza hisa zao kwa kampuni ya Kitanzania Highland Estates Ltd.

Highland Estates Ltd nayo ilifuatilia hati bila mafanikio. Iliwekeza kiasi cha dola laki nane za Kimarekani (US$ 800,000).

Highland Estates Ltd iliposhindwa kupata hati, mwaka 2000 nayo iliuza hisa zake kwa kampuni nyingine ya Kitanzania AFRIKA MPYA LTD.

Wakati wote huo MIM (kampuni ya wafanyakazi) ilikuwa bado ipo palepale na hisa zao asilimia 10.

**MZOZO WA PSRC, KATANI NA USULUHISHI**

(AFRIKA MPYA na MIM) wakiwa kama KATANI Ltd iliendelea kufuatilia upatikanaji wa hati na ilipofika Februari 2002 Katani na PSRC walifikishana mbele ya wasuluhishi wa mgogoro huo kama ilivyoelekezwa kwenye mkataba.

Wasuluhishi katika mgogoro huo walikuwa Wanasheria Marehemu Mzee Peter Bakilana (Wakili wa Kujitegemea), Mwenyekiti Mheshimiwa Mzee Joseph S. Warioba (Waziri Mkuu Mstaafu)– Mjumbe na Mzee Mohamed Ismail (Wakili wa Kujitegemea) - Mjumbe



*Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akipokea taarifa kutoka kwa Mwenyekiti wa Kamati Maalum aliyoiunda ya kuchunguza zao la mkonge, Gerlad Kusaya baada ya taarifa hiyo kusomwa mbele ya Waziri Mkuu katika kikao kati ya Waziri Mkuu na watumishi na viongozi wa Halmashauri za Mkoa waTanga kilichofanyika kwenye ukumbi wa hoteli ya Naivera jijini Tanga, hivi karibuni.*



Mwenyekiti wa TPSF, Salum Shamte.

**YALIYOBAINIKA**

Katani ililipa mikupuo miwili ya bei ya mauzo ya mali za MGC kama ilivyotakiwa kwenye mkataba;

Katani ilitekeleza baadhi ya vipengele vilivyo kwenye Mpango wa Biashara (Business Plan), ambao ulikuwa ni sehemu ya mkataba;

Katani haikuharibu na ililinda mali na miundombinu iliyokarabatiwa, kinyume na madai ya PSRC;

Katani haikukiuka haki za Serikali kama PSRC ilivyodai.

HUKUMU

Ilielekeza Katani waingie makubaliaano upya na Serikali. Hii ilipelekea Katani na Serikali kutengeneza na kutiliana saini Hati ya Makubaliano (Memorandum of Understanding), Aprili 2005 na kusaini Mkataba Mpya Machi 2007, ULIOTHIBITISHA KATANI LTD HAIDAIWI NA SERIKALI.

**KUINGIZWA WAKULIMA WADOGO NA WA KATI**

Katani Ltd iliasisi mfumo wa Wakulima Wadogo wa mkonge kuanzia mwaka 2000, ili kupanua milki ya mashamba ya mkonge. Mfumo huo ulifanikiwa kwa kiasi kikubwa sana.

Kwa kuwa Katani ilipewa baadhi tu ya hati mwaka 2005; iliona badala ya kung'ang'ania hati iwashirikishe wananchi wengine 2,100 ambao wengi walikuwa wafanyakazi katika mashamba hayo, na kuwaendeleza ili wawe Wajasiriamali Vijijini;

Kila kaya ya hao wananchi 2,100 pamoja na wote wa MIM, walipewa eka 15 bure.

Serikali ilitoa hamasa kubwa sana iliyosababisha watu wengi kujitokeza kuchukua mashamba hayo.

Masharti ya mashamba hayo ni kwa kila mkulima kulima mkonge ingawa katikati ya miraba walilima mazao ya chakula.

**USHIRIKI WA NSSF KWENYE KATANI LTD**

Katani Ltd ilitambua kuwa wengi wa wakulima wadogo hawana uwezo wa kuendeleza mashamba hayo. Lakini hata wakulima wa kati hawakuwa na uwezo hasa ukitilia maanani zao la mkonge linalochukua miaka mitatu kabla kuanza kuvunwa.

Kwa mantiki hiyo, Katani Ltd iliomba ushiriki wa NSSF ili watoe mkopo kwa kuendeleza kilimo cha mkonge.

Ili kukidhi mahitaji ya mpango mzima wa miaka kumi (10) wa Biashara, Katani Ltd iliomba mkopo wa dola za Kimarekani milioni sabini. NSSF ilikuwa iungane na mashirika mengine ya fedha ili kufanikisha mkopo huo.

NSSF, kama ilivyo mifuko ya jamii / pensheni ulimwenguni ndiyo chanzo kimoja kikuu cha kukuza uchumi na inatumika duniani hasa kwa mikopo ya muda mrefu.

Kwa bahati mbaya sana NSSF haikufanikiwa kupata fedha zilizohitajika za mpango wa miaka kumi wa biashara wa Dola za Kimarekani milioni sabini (70).

Waliweza kutoa sehemu ndogo sana ya kiasi cha Dola za Kimarekani milioni sita na laki saba.

NSSF walikubali kwa masharti kuwa Katani watoe mkopo huo kwa wakulima kwa njia ya huduma nne, za kuwalimia, kuwapandia mbegu bora, kuwapa utaalamu, kuwasaidia upatikanaji wa masoko.

**MKOPO WA NSSF ULIVYOGAWANYWA**

Ununuzi wa vifaa kama matrekta, mabuldoza, makatapila, mashine za uendeshaji wa mashamba, viwanda na uendeshaji kwa Katani Ltd.

Kadhalika, ilielekezwa malipo kutoka kwa wakulima yatakatwa watakapoanza kuvuna na kulipwa;

**UFANISI WA MKOPO**

Uzalishaji ulipanda kutoka Tani 849 mwaka 2005 mpaka Tani 5,420 mwaka 2017.

Katani Ltd iliweza kukarabati viwanda vitatu na kujenga viwanda vipya vinne vya kusindika mkonge katika wilaya ya Korogwe ambavyo awali vilikuwa vimekufa kwa zaidi ya miaka 15.

Katani ilijenga kiwanda cha kwanza duniani cha kuzalisha umeme kutoka kwenye mabaki au takataka za mkonge ambazo awali zilikuwa zinatupwa tu – (FIRST IN THE WORLD SISAL ENERGY PLANT AT HALE ESTATE).

Katani iliweza kukarabati na kùpanua kiwanda cha Tancord cha kuzalisha bidhaa za mkonge.

Katani iliweza pia kutoa gawio kwa wanahisa mwaka 2013, 2014 na 2015.

**NSSF KAMA WANAHISA**

NSSF waliona upungufu mkubwa wa mahitaji ya fedha zaidi kwa Katani Ltd kama walivyoomba awali.

Hii ilitokana na wananchi zaidi kutaka kuingia kwenye mradi, ikiwa ni pamoja na wahariri wa baadhi ya vyombo vya habari ambao walifanya kazi nzuri sana ya kuhamasisha wananchi.

Wananchi waliona mabadiliko mazuri ya wenzao walioko kwenye mradi wanavyoweza kuyakabili maisha.

**NSSF ILIKUBALI HAYA**

NSSF ilibadilisha mkopo wa kwanza wa dola milioni 6.7 kuwa hisa na walikubaliana hisa asilimia 49.

Pia walikubali kutoa mkopo wa ziada kukidhi ongezeko la mahitaji.

**MASHARTI YA NSSF**

NSSF walitaka Mwenyekiti wa Bodi ya Katani Ltd, ateuliwe na NSSF na mjumbe mmoja mwingine wa Bodi.

NSSF ishiriki kumteua Mkurugenzi mpya wa Fedha na walishiriki kumteua Fadhili Mhina kama Mkurugenzi wa Fedha wa Katani Ltd.

NSSF ifanye ukaguzi wa Katani Ltd kila miezi 6, isitoshe, ilikubaliwa kwamba Meneja Mwandamizi kutoka idara ya Mipango na Uwekezaji ya NSSF atakuwa anahudhuria mikutano yote ya Bodi ya Katani ambapo atapata taarifa ya maendeleo ya miradi inayotekelezwa kwa fedha za mkopo kutoka NSSF.

**MAAGIZO YA RC TANGA**

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Martin Shigela maagizo yake yanadaiwa kusababisha kushuka kwa utendaji wa Katani Ltd kwani alileta vikwazo vingi kwa kampuni.

Kibaya zaidi aliifungia kwa nguvu Katani Ltd isizalishe kwenye viwanda vyake vyote kwa muda wa miezi sita mwaka 2018.

Huu ni muda mrefu sana kwa kampuni kubwa kama Katani kufungiwa.

Alielekeza mkonge wote uuziwe kampuni ya Kichi pekee.

Kiwanda cha TANCORD kilinyimwa mkonge hata uliokuwa unatoka kwenye mashamba ya wanahisa, alielekeza pia auziwe Mchina ambaye mkonge wote alikuwa anaupeleka China.

Kiwanda cha Katani ambacho ni cha kwanza kwa ukubwa Afrika, kiliporomoka na kuzalisha asilimia 20 tu kwa kukosa mali ghafi.

Kiwanda kilipunguza wafanyakazi kufuatana na uzalishaji.

Serikali ilikosa kodi mbalimbali kwani Katani Ltd ni mmoja kati ya walipaji wakubwa wa kodi mkoani na mauzo ya nje ya takriban shilingi bilioni 10.

Katani Ltd Septemba 3 2018 ilimwandikia barua Mkuu wa Mkoa yenye kichwa cha habari "ATHARI ZA MAAGIZO YA KIKAO CHAKE CHA AGOSTI 2018 NA KUORODHESHA ATHARI ZOTE NA USHAURI".

Katani Ltd bado wanasisitiza kuangaliwa upya maagizo hayo ambayo kimsingi yanaua zao la mkonge Tanzania na tutakuja juta.

Menejimenti na Wafanyakazi wa Katani Ltd wamekuwa kwenye soko la mkonge kwa zaidi ya miaka hamsini (50), na inazijua mbinu zote ambazo zinaweza kutumika ikiwemo bei, upatikanaji, n.k ambazo zitalenga kwenye kuididimiza sekta ya Mkonge Tanzania.

**MKOPO KWA TPI**

Kampuni hizi mbili, Katani Ltd na Tanzania Pharmaceutical Industries Ltd (TPI) ni Kampuni binafsi (Private Companies), ambazo zina mamlaka kamili ya kukopa na kukopesha, kushtaki na kushtakiwa. Ndio maana Katani Ltd iliweza kukopa popote ilipokubalika.

Kampuni nyingi binafsi (Private Companies) zina utaratibu wa kukopeshana, iwe fedha na/au malighafi.

Kwa mantiki hiyo, Katani Ltd ilipokuwa na ukata na kukosa fedha za kuendeshea mkutano wa Kimataifa wa Nyuzi Ngumu Asilia (International Conference on Hard Natural Fibres), Salum Shamte alikuwa Mwenyekiti wa "FAO Conference on Hard Fibres.

Mkutano huo ulifanyika Tanga, Tanzania, hivyo Katani iliomba mkopo kutoka TPI. TPI iliikopesha Katani Ltd fedha hizo. Mkutano ukafanyika na Katani ilipokuwa na ukwasi, walizirejesha fedha hizo.

Kadhalika TPI ilipopata dharura na kuhitaji kile kinachoitwa "bridging finance", iliomba mkopo kutoka Katani Ltd.

Katani Ltd ilitoa mkopo huo kwa TPI kwa riba ya asilimia kumi na sita (16%). TPI iliurejesha mkopo huo wote, ikiwa ni pamoja na riba.

Uhusiano huu ulikuwa ni wa kibiashara na pande zote mbili zilinufaika. Na hiyo ndio biashara.

**NYUMBA YA LONDON**

Tuhuma zimeelekezwa kwa Shamte kwamba aliuza nyumba (na pesa kutia mfukoni mwake), mali ya Mamlaka ya Mkonge Tanzania, iliyoko London na ambayo alikuwa akiishi alipokuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Tanganyika Sisal Marketing Association (TASMA); Kampuni tanzu ya Tanzania Sisal Authority (TSA).

Ukweli ni kwamba, nyumba hiyo ya London ipo Edgware na Shamte alipoondoka aliiacha mikononi mwa Ubalozi wa Tanzania.

Ushahidi upo na haingii akilini kwa nini "TUME" ilishindwa kuwasiliana na Ubalozi wa Tanzania nchini Uingereza na kupata ukweli.

**NYUMBA YA TANGA**

Nyumba ya Shamte anayokaa Tanga aliuziwa wakati wa Ubinafsishaji, miaka ya 1990/2000. Mauzo haya yalifanyika kihalali kama yalivyofanyika kwenye nyumba nyingine za Mashirika ya Umma yaliyo binafsishwa kama vile Benki ya Taifa ya Biashara (NBC), Tanzania Breweries Limited, Tanzania Cigarette Company Limited, SIMU 2000.

Isitoshe, kuna nyumba nyingi ziliuzwa kwa wafanyakazi wa Serikali na Mashirika ya Umma waliokuwa wanaishi kwenye nyumba hizo.

Ni vigumu kuamini kama Serikali ina nia ya kuwanyang'anya maelfu ya nyumba zao walizouziwa kihalali kutokana na maamuzi sahihi ya Serikali ya wakati huo.

MWISHO

Kwa kuwa taarifa ile ilisomwa kwa umma, basi umma lazima upate taarifa ya upande wa pili, ili uwe kwenye nafasi nzuri ya kupambanua kati ya HAKI na BATILI.

Haki sio tu inatakiwa itendeke, bali inatakiwa ionekane kuwa inatendeka. Ni muhimu Shamte na wenzake wapewe fursa ya kujibu tuhuma zilizoelekezwa kwao na "Tume" ya uchunguzi.

**Mwandishi wa makala haya ni mdau na mkulima wa Mkonge, Tanga.**



*Shamba la mkonge*

Scanned with CamScanner